



# Huduma za Msaada wa Mpito kwa Vijana

## MABADILIKO KWA HUDUMA KUTOKANA NA COVID-19

Msaada chini ya Huduma za Msaada wa Mpito kwa Vijana unaendelea kupatikana kwa wateja wakati wa mlipuko wa COVID-19. Hata hivyo, njia ambayo huduma zinawasilishwa inaweza kubadilika kulingana na ushauri rasmi wa afya.

Badala ya kukutana uso kwa uso au vikao vya kikundi, mawasiliano ya mtu binafsi na wateja sasa yanafanywa kwa simu na watoa huduma wanafanya kazi wa kikundi kupitia majukwaa tofauti ya mitandao ya kijamii ikiwa ni pamoja na zoom, WhatsApp na Facebook.

Watoa huduma wanaweza kutumia huduma za ukalimani kwa simu kwa wateja ambao hawaongei vizuri Kiingereza.

Jifunze kuhusu [\*\*COVID-19 na dalili zake \(symptoms\)\*\*](#).

## Nini maana ya Huduma za Msaada wa Mpito kwa Vijana (YTS)?

Huduma za YTS husaidia vijana wahamiaji wa kibinadamu na wahamiaji wenye hatari kati ya miaka 15 hadi 25 ili kushiriki katika kazi na elimu, kuboresha utayari wao kwa mahali pa kazi, kutoa upatikanaji wa fursa za masomo ya kazi, na kujenga uhusiano imara wa kijamii kupitia elimu na ushiriki wa michezo.

Vijana wa kibinadamu na wahamiaji wengine wanaweza kukumbana na changamoto katika kupata huduma za usaidizi, kuweza mahitaji ya mafunzo na kujiweka wenyewe kwa ajira, na mara nyingi wanahitaji msaada wa ziada ili kupata na kuendeleza na uhusiano katika jamii yao mpya.

Hii inaweza kuwa kutokana na vizuizi vya lugha na utamaduni, na/au ukosefu wa mitandao imara na maarifa ya soko la ajira za eneo hilo.

Familia za vijana nazo pia zinaweza kupambana na masuala ya uhusiano na mahusiano ya kijamii.

Huduma za YTS zinawasilishwa na watoa huduma kupitia miradi mbalimbali na shughuli ikiwa ni pamoja na kuwasaidia vijana kuungana na huduma za ajira za eneo hilo na kazi, na elimu zaidi ya ufundi au nyingine.

## Ni namna gani huduma ya YTS inasaidia vijana?

Huduma za YTS husaidia kujenga uwezo na ustahimilivu miongoni mwa washiriki vijana wa kibinadamu na wahamiaji wengine stahifu ili kuwasaidia kuendelea kushiriki katika elimu na kufanya mabadiliko ya mafanikio kwa ajira.

Huduma za YTS hulenga maeneo manne muhimu. Hayo ni:

- Ushirikiano wa aAira ili kuboresha utayari wa kazi wa vijana.

- Miunganisho mikali ya elimu ili kusaidia vijana kukaa pamoja na elimu.
- Fursa za mafunzo za kuwasaidia vijana kupata na kuimarisha ujuzi wao wa amali.
- Ushirikiano wa michezo ili kuwasaidia vijana kujenga uhusiano wa kijamii na imani kupitia mipango ya michezo.

## Je ninastahili kupokea huduma hizi?

Unaweza kuwa na haki ya kupata huduma za YTS ikiwa wewe ni mkaazi wa kudumu wa umri wa miaka kati ya 15 hadi 25 na uliwasili nchini Australia katika miaka mitano iliyopita kama mhamiaji wa Kibinadamu, au viza ya kuungana na Familia ukiwa pia na uwezo mdogo wa Kiingereza.

## Naweza kupata huduma za YTS namna gani?

Jedwali chini linaorodhesha watoaji huduma wanaotoa huduma ya YTS. Ikiwa una nia ya kushiriki katika programu, tafadhali wasiliana na mtoa huduma hapa chini katika eneo lako la ndani.

Mtoa huduma	Huduma za YTS zinapatikana katika maeneo yafuatayo
Lebanese Muslim Association	Canterbury, Bankstown, Liverpool and Fairfield, NSW
Community Migrant Resource Centre Inc (Parramatta)	Auburn and Blacktown, NSW
Multicultural Australia	Brisbane, QLD
Access Community Services Limited	Logan, QLD
Victorian Foundation for Survivors of Torture Inc (Foundation House)	Greater Dandenong, Casey, Hume, Brimbank, Darebin, Maribyrnong, Melbourne and Whitehorse, VIC
Brotherhood of St Laurence	Hume, VIC